

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
13 Desemba 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Bashiri Rashidi  
Beda John Mkusu  
Canon Mallicia  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rwechungura  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Idrisa Kessi Zongo  
Juma Ali Salehe Jongo  
Kibwana Mohammad Msiga  
Mohamedi Saidi  
Shamte J Kigoma  
Solomon Mihoyo  
Sudi Saidi Ramadhan

Wageni

Johannes Warn - TASEA

Olive Lyimo - TASEA

**TASEA**

Wageni kutoka TASEA walieleza kwamba TASEA - Tanzania Solar Energy Association – ni NGO imanza 2001 na ina wanachama 250 ambao ni watu wanaopendelea nishati jadidifu / nishati endelevu. Wanachama ni watu binafsi, biashara na watafiti. Serekali ya Ujerumani ina mradi wa volunteer kwa vijana na sasa Johannes ni volunteer kwa TASEA chini ya mradi huu. UWABA tulisema sisi tungependa kuwa na volunteer – ataweza kusaidia katika kuongea na serekali kuhusu masuala ya baisikeli, kusaidia kuandaa matukio ya UWABA, kufundisha kompyuta kwa wanachama na kusaidia kuanzisha shirka la courier ya baisikeli Dar es Salaam.

**Repoti ya msafara**

Elaine alileta nakala za repoti ya msafara. Filbert atapeleka nakala kwa kampuni ya Guta wiki hii.

**Mradi wa Wamba**

Elaine alichapa repoti ambayo Filbert aliandika, na Filbert alisahihisha. Elaine atatafsiri na ataweka kwenye website na atatumia kwa Wamba memorial fund.

**Video ya usalama barabarani**

Elaine hajapata nafasi ya kuweka kwenye DVDs – atafanya wiki hii.

**Mkutano na serekali ya jiji**

Filbert alipeleka barua kuomba mkutano na serekali ya jiji Jumatano. Alizunguka kwenye maofisi mbali mbali ndani ya ofisi ya serekali ya jiji na aliambiwa arudi Ijumaa. Aliporudi Ijumaa barua haijaenda kutoka utawala mpaka mtu anayehusika na alifuatalia. Atafuatalia tena Jumatatu.

**Mkutano na Foundation for Civil Society**

Elaine alitumia email kwa Foundation for Civil Society kuomba mkutano, lakini hawakujibu. Atawapigia simu wiki hii.

**Wizara ya Miundombinu**

Elaine aliandika barua kwa wizara ya miundombinu kuomba UWABA tuwe kwenye orodha ya washika dau. Idrisi atapeleka wiki hii.

**Mambo mengine**

Bashiri aliomba samahani ya text message alitumia kwa Elaine ambayo inaonekana hatafanya kazi yoyote bila posho, lakini hakutegemea iwe na maana kama hivyo.

Juma alisema kwamba hela ya guta Tsh 35,000 inadaiwa.

Hamadi Bwaja aliomba kitambulisha mpya

.